

Toleo la. 15

Jarida la *Ni Magufuli Tena*

2020 - 2025

ALIAHIDI | AMETEKLEZA | APEWE TENA 5 | 14 SEPTEMBER, 2020



MAGUFULI ATIKISA CHATO



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**

TAHARIRI

VIYAMA VYA SIASA HUBIRINI AMANI SIO MACHAFUKO

Wakati kampeni za kugombea za Urais, Ubunge na Udiwani katika Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28, 2020, baadhi ya wanasiasa wamekuwa wakinadi Ilani za vyama vyao huku wakitoa matamshi yenye viashira vya uvunjifu wa amani nchini Tanzania.

Ikumbukwe kuwa amani ya nchi yetu haikuja hivi hivi tu bali ilijengwa na kuenziwa na Awamu zote za uongozi wa nchi hii na hata sasa Serikali ya Awamu inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli imeendelea kusimamia na kuimarisha amani ambayo ni tunu muhimu kwa watanzania

Ustawi wanachi yeyote duniani unategemea uwepo wa amani. Tanzania ya leo ambayo imepiga hatua kubwa kimaendeleo ikiwemo ujenzi wa miundombinu muhimu inayowawezesha watanzania kufanya shughuli za kiuchumi, ni kwa sababu kumekuwa na amani tofauti na nchi nyingine ambazo zina rasilimani nyingi lakini wananchi wake wapo katika wimbi la umasikini kwa sababu tu hakuna amani.

Tunatoa wito kwa baadhi ya vyama vya siasa ambavyo vimeanza kujipambanua kuwa na ajenda ya kutaka kusababisha machafuko badala ya kuhubiri amani, kuacha mara moja kwani amani haina mbadala zaidi ya kuwapa mateso wananchi na kulirudisha Taifa nyuma kimaendeleo.

Aidha, tunapenda kukipongeza Chama cha Mapinduzi pamoja na wagombea wake katika nafasi za Urais, Ubunge na Udiwani kwa kusisitiza amani ikiwemo kuwaalika viongozi wa dini katika mikutano ya kampeni ili walioombe Taifa lipitite salama katika safari ya kuelekea Uchaguzi Mkuu unaotarajiwa kufanyika Oktoba 28 mwaka huu.

Amani ya Tanzania ni muhimu kuliko vyama vya siasa. Ustawi wa watanzania unategemea uwepo wa amani, hivyo ni jukumu la kila mtanzania kutumia fursa ya Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu kuchagua viongozi wachapa kazi, waadilifu na wanaohubiri amani badala ya wale wanaohamasisha vurugu.



A photograph of President John Pombe Magufuli of Tanzania. He is an older man with glasses, wearing a blue button-down shirt. He is seated in a wooden chair with a red upholstered back. The background is a bright yellow wall. Other people are partially visible in the background, some in military uniforms.

MAGUFULI: WATANZANIA TULINDE AMANI YETU

Na Mwandishi Maalum - **GEITA**

Mgombea Urais kupitia Chama Cha Mapinduzi (CCM) na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli, amewaasa watanzania kulinda tunu za amani, umoja na mshikamao uliopo hapa nchini ili kuchochea zaidi maendeleo yaliyofikiwa katika kipindi chote tangu Taifa lipate uhuru.

Rais Magufuli amesema hayo leo katika uwanja wa Mazaina mjini Chato mkoani Geita katika mkutano wa kampeni za Urais, Ubunge na Udiwani kwa Muhula wa Pili wa Awamu ya Tano ambapo amesema Tanzania imekuwa nchi ya amani ambayo watu wanafanya biashara zao, wanaabudu na kutembea kwa uhuru.

“Ila huu uhuru usije ukawalevya, msicheze na kukosekana kwa amani kwani majuto yake ni makubwa. Ninawaomba watanzania tusimame imara bila kubaguana huku lengo likiwa moja la kujenga nchi yenye maendeleo, uchumi na yenye kusimamia usalama na maadili ya watanzania wote”, amesisitia Dkt. Magufuli

Sambamba na hilo, amevishukuru vyombo vya ulinzi na usalama kwa kusimamia amani na usalama wa nchi kwa kudhibiti changamoto za kiusalama zilizojitokeza mwanzoni mwa uongozi wake.

“Ilifikia wakati kuna sehemu ilikua wananchi ili waweze kufika lazima wasindikizwe na polisi, tukasema hapana, majambazi hawawezi wakatawala katika nchi hii ndio maana navipongeza sana vyombo vya ulinzi kwani nchi ikikosa amani na usalama basi hakuna maendeleo.” alieleza Rais Dkt. Magufuli.

Pamoja na hayo, amesema vyombo vya ulinzi na usalama vimeiwezesha Tanzania kuwa nchi ya maana miongoni mwa Mataifa mengi duniani na kuwataka wananchi wasikubali kupotoshwa na watu wenye nia ya kuwagawa watanzania na kuleta mfarakano nchini.

Kwa mujibu wa Global Peace Index 2020, Tanzania ni moja ya mataifa yanayoongoza kwa amani barani Afrika huku ikishika nafasi ya kwanza Afrika Mashariki.



VIONGOZI WA DINI WALIOMBEA TAIFA AMANI, UTULIVU

Na Mwandishi Wetu - **GEITA**

Viongozi wa dini nchini wamemuomba Mwenyezi Mungu aiwezeshe Tanzania kumaliza Uchaguzi Mkuu kwa amani na utulivu.

Akisoma dua ya kwenye ufunguzi wa mkutano wa kampeni wa CCM leo mjini Chato, mkoa wa Geita, Sheikh wa Mkoa, Alhaji Yusufu Kabaji alimuomba Mungu akisema aendeleo kuisimamia amani ya nchi. "Taifa letu limekuwa kisiwa cha amani, hivyo tunakuomba Mola wetu utuwezeshe uchaguzi wetu upite kwa amani na utulivu," amesisitiza.

Amani hiyo iliyodumu nchini inatokana na uadilifu wa Viongozi Wakuu wa nchi, hali iliyochangia kuleta maendeleo katika sekta mbalimbali.

"Tunakushukuru Mungu kwa kazi ambayo Rais Magufuli amefanya katika kipindi cha miaka mitano iliyopita na utujalie kupata viongozi watakaotuongoza kwa uadilifu," alisema Askofu Mkuu wa Kanisa la Africa Inland church (AIC), Mussa Magwesele katika sehemu ya maombi yake

Sambamba na hayo, Mosinyori, Henry Mlinganisa wa Kanisa Katoliki Jimbo la Rulenge, Ngara amemuomba Mungu ambariki Rais Magufuli.

"Mungu tunakuomba uzidi kumjalia baraka Rais wetu, Dkt. Magufuli, utujalie uchaguzi wenye heri na amani na pia uwariki wote walio hapa na uwajalie kucha-gua kiongozi kwa kadiri ya mapenzi yako," aliomba Mlinganisa.



ILANI: AJIRA ZITOKANAZO NA VIWANDA KUONGEZEKA MARA DUFU

Na Mwandishi Wetu

Serikali itaendeleza mafanikio yaliyopatikana katika kipindi cha miaka mitano iliyopitana kubuni mikakati zaidi ili kujenga uchumi wa viwanda jumuishi, fungamanishi na shindani vinavyotumia malighafi za ndani. Kwa mujibu wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025, viwanda hivyo vitatumia teknolojia ya kisasa na vitakidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi hivyo kuzalisha ajira zaidi na kukuza uchumi.

“Lengo katika kipindi cha mwaka 2025 ni kuongeza ajira zitokanazo na uzalishaji wa bidhaa viwandani kutoka 306,180 mwaka 2020 hadi 500,000 mwaka 2025 ambapo malighafi zinazotumika zitakuwa za ndani hasa zinazotokana na kilimo, mifugo, maliasili na madini”, inasisitiza sehemu ya Ilani.

Aidha, Ilani hiyo inaeleza kuhusu kuendelezwa na kujengwa viwanda mama ikiwemo viwanda vya Chuma Liganga na Mchuchuma, Madawa na kemikali (Magadi Soda Engaruka) ambavyo vitaleta faida nyingi kwa Taifa ikiwa ni pamoja na ajira, uongezaji thamani malighafi za ndani, uanzishwaji viwanda vingine, na kupanua shughuli katika sekta za ujenzi na miundombinu. Pia, Ilani inatilia mkazo kufungamaisha ujenzi wa kanda maalum za viwanda na biashara, na kutumia miundombinu ya kimkakati iliyopo na itakayojengwa ikiwemo Reli ya Kisasa (SGR), Reli ya Kati, TAZARA, Bandari kavu na upanuzi wa barabara.

Hatua nyingine itakayochukuliwa katika Muhula wa Pili wa Serikali Awamu ya Tano ni kuweka utaratibu wa kuendelea kufuatilia viwanda vilivyobinafsishwa ili kuhakikisha vinafanya kazi kwa malengo yaliyokusudiwa na hivyo kuongeza ajira na uzalishaji wa bidhaa nchini.

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Serikali ilifanikiwa kuongeza viwanda vipya 8,477 na kufanya idadi ya viwanda kufikia 61,110 kati ya viwanda hivyo vipya 201 ni vikubwa, 460 vya kati, 3,406 vidogo na 4,410 vidogo sana, kwa kiasi kikubwa viwanda hivi vinatumia malighafi za ndani na kuajiri wananchi wengi.

A photograph of Mhe. Samia Suluhu Hassan, the Vice President of Tanzania, speaking into a microphone. She is wearing a black hijab, sunglasses, and a bright green patterned long-sleeved shirt. She is gesturing with her right hand while holding the microphone in her left. The background shows a clear blue sky with some clouds, palm trees, and a flagpole with a Tanzanian flag.

MAGUFULI KUKUZA KILIMO-BIASHARA RUVUMA

Na Mwandishi Maalum - RUVUMA

Mgombea Mwenza wa Urais kupitia Chama cha Mapinduzi (CCM) Mhe. Samia Suluhu Hassan, amesema Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Pombe Magufuli imepanga kufanya uwekezaji wa kilimo-biashara mkoani Ruvuma kwa kujenga maghala makubwa yatakayokuwa na uwezo wa kuhifadhi tani 531,880 za mazao.

Mpango huo pia utawasaidia wakulima kuzalisha mazao bora ambayo yataongeza soko na hatimaye kuwa na uhakika wa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara.

Mhe. Samia ameyasema hayo leo alipohutubia mkutano wa Kampeni uliofanyika kwenye uwanja wa Taifa wa Lwinda, wilayani Namtumbo mkoani Ruvuma ambapo amesema kwamba hatua ya Serikali ya CCM kujenga maghala hayo, pia itawafanya wakulima kuwa na ari ya uzalishaji mashambani.

"Kwenye kilimo tutaongeza miundombinu ya umwagiliaji, najua hapa Namtumbo mnayo skimu ya umwagiliaji, pia tutaongeza uwekezaji wa kilimo-biashara kwa kujenga maghala makubwa ya kuhifadhi mazao ya chakula cha wastani wa tani 531,880, lengo ni kufanya tuwe na chakula kingi na kuwapa motisha wakulima kwani uwepo wa maghala hayo ni soko la uhakika," amesema.

Sambamba na hayo, Samia pia amesema Serikali ya Magufuli imepanga kuboresha chanzo kikubwa cha maji Matogoro wilayani humo ili kuwapatia wakazi wake maji Safi na salama wakati wote. "Kuhusu Mkoa wa Ruvuma Kazi kubwa imefanyika, tunatekeleza miradi mikubwa 82 na mingine 33 ipo katika hatua ya utekekezaji. Kwa vijiji ambavyo bado havi-japata maji, tutahakikisha mpaka kifikia mwakani vyote vitakuwa na maji," aliwahakikishia wananchi wa Namtumbo.

Akizungumzia uwezeshaji wananchi kiuchumi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita, Mhe. Samia amesema zaidi ya bilioni 4.3 zimekopeshwa kwa vijana, wanawake na wale-mavu mkoani Ruvuma ambapo kwa wilaya ya Namtumbo pekee shingi milioni 236 zime-tolewa kwa makundi hayo.



CCM: MIHULA YA URAIS ITABAKIA KUWA MIWILI TU

Na Mwandishi Wetu - **GEITA**

Chama Cha Mapinduzi (CCM) kimewataka wananchi kupuuza uzushi unaodai eti Chama hicho kina mpango wa kuongeza muda wa uongozi kwa kiti cha Urais kutoka mihula miwili hadi mitatu kwa awamu moja hivyo kuiwezesha Serikali ya Awamu ya Tano kudumu kwa miaka 15.

Kauli hiyo imetolewa na leo mjini Chato na Katibu Mkuu wa CCM, Dkt. Bashiru Ali alipofungua mkutano wa kampeni uliofanyika katika uwanja wa Mazaina mjini humo ambapo amesema amelazimika kutoa taarifa hiyo kufuatia upotoshaji unaoendelea katika mitandao ya kijamii.

“Kuna upotoshaji unaendelea mitandaoni kuwa Chama cha Mapinduzi kinafanya jitihada za kushinda viti vingi vya ubunge katika uchaguzi mkuu ujao ili kibadili utaratibu na kumuongeza muda wa kiti cha Urais kwa kipindi cha tatu baada ya kipindi cha pili cha Serikali ya Awamu ya Tano kukamilika, taarifa hizi si za kweli hivyo naaomba zipuuzwe”, alieleza Dkt. Bashiru

Dkt. Bashiru amefafanua kwamba wanasiasa wanaozusha taarifa hizo wamefilisika kisiasa na hawana agenda hivyo wamejikuta wakizusha mambo yasiyo na ukweli.

Kuhusu kampeni za Chama hicho, amesema zinaendelea kwa kasi na mafanikio huku akibainisha kuwa wajumbe wa Kamati za siasa katika ngazi zote wanafanya kazi nzuri katika kuhakikisha kampeni za kuomba kura kwa wananchi zinafanikiwa kwa kiwango cha juu na kwamba Chama kinapata uungwaji mkono mkubwa.

Aidha, Dkt. Bashiru alimpongeza mgombea wa Chama hicho na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ikiwemo ya kuwezesha utekelezaji wa mradi mkubwa wa bomba la mafuta kutoka Hoima, Uganda hadi Chongoleani, Tanga.

Mgombea Urais kupitia CCM anaendelea na kipindi cha pili cha kampeni za kuomba kura baada ya kukamilisha kipindi cha kwanza kilichohusisha mikoa ya Dodoma, Singida, Shinyanga, Simiyu, Mara, Mwanza na Geita.

5 KALI ZA MAGUFULI WILAYANI CHATO

Amani, Utulivu, Mshikamano, Ulinzi na Usalama,

01

Navishukuru sana vyombo vya ulinzi na usalama kwa kusimamia amani na usalama wa Taija letu, wakati naingia madarakani ilifika hatua hasa kule Kibiti watu waliuawa kwa kupigwa risasi ndio maana tulisimama imara kwamba ulinzi na usalama katika nchi yetu ni kipaumbele namba moja.

02

Ilifikia wakati kuna sehemu wananchi kufika lazima wasindikizwe na Polisi, tukasema hapana majambazi hawawezi wakatawala katika nchi hii ndio maana navi-pongeza sana vyombo vya ulinzi kwani nchi ikikosa amani na usalama basi hakuna maendeleo.

03

Vyombo vya Ulinzi na Usalama vimefanya kazi kubwa, vimeiwezesha Tanzania kuonekana nchi ya maana miongoni mwa Mataifa mengi duniani, kamwe msikubali watu wanaokuja kutugawa na wanaojifanya wanaijua Tanzania.

04

Tanzania imekuwa nchi ya amani, watu wanafanya biashara zao, wanaabudu na kutembea kwa uhuru ila huu uhuru usije ukawalevya, msicheze na kukosekana kwa amani kwani majuto yake ni makubwa. Ninawaomba Watanzania tusimame imara bila kubaguana huku lengo likiwa moja la kujenga nchi yenye maendeleo ya uchumi na yenye kusimamia usalama na maadili ya Watanzania wote.

05

Tunaitengeneza nchi kuwa nchi ya kisasa, sijamuona mgombea mwingine yeyote wa Urais ambaye anaweza kutekeleza hata robo tu. Lazima niwaambie ukweli kama mnataka kujaribu jaribuni siku moja mtaniambia.



BILIONI 73 KUKARABATI MADARAJA, BARABARA RUVUMA

Na Mwandishi Mahususi - RUVUMA

Serikali imetoa shilingi Bilioni 73.7 kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa madaraja na barabara mkoani Ruvuma, ili kufungua fursa za kiuchumi kwenye Mikoa ya Kusini mwa Tanzania na nchi jirani.

Barabara zitakazohusika katika mpango huo ni zile zinazounganisha barabara za Mkoa huo na mikoa mingine pamoja na nchi jirani zinazopakana na Ruvuma.

Akizungumza katika mkutano wa Kampeni uliofanyika kwenye uwanja wa Ndege uliopo katika kijiji cha Nanjoka wilayani Tunduru mkoani Ruvuma, Mgombea Mwenza na Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Samia Suluhu Hassan, amesema Serikali ina malengo makubwa na Mkoa wa Ruvuma na kuwaomba wakazi hao kumchagua Dkt. John Pombe Magufuli ili aendeleeze ujenzi huo wa Barabara.

"Tumetoa shilingi bilioni 73.7 za ujenzi wa miradi ya barabara, tunaufungua mkoa wa Ruvuma kiuchumi. Mkoa huu una umuhimu mkubwa hivyo mchagueni Dkt. John Pombe Magufuli ili aendeleeze ujenzi wa miundombinu katika mkoa wa Ruvuma na Tanzania kwa ujumla," alieleza Samia.

Aidha amesema Serikali pia inaendelea kuimarisha na kuzipa nguvu Wakala zake mbili ikiwemo ya usimamizi wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA) na Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD) ili kuendelea kujenga Barabara nyingi zaidi.

Samia pia amezungumzia ahadi yake ya upatikanaji wa maji Safi na salama katika wilaya ya Tunduru ambapo amesema zaidi ya milioni 196 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi wa miradi ya maji Wilayani humo.

Wananchi wa wilaya ya Tunduru inayopakana na Hifadhi ya Taifa ya Selous, wamemueleza Mgombea Mwenza huyo kuwa wanakabiliwa na changamoto ya wanyamapori hasa Tembo katika vijiji wanavyoishi ambapo Mhe. Samia amewaeleza kuwa tayari Serikali imeanza kutafuta ufumbuzi wa changamoto hiyo.

"Suala la uvamizi wa wanyamapori tumeanza kulishughulikia, hapa Tunduru kulikuwa na kikosi kimoja tu cha kulinda wanyamapori wasiathiri binaadamu na mali zao. Tumeongeza vikosi vingine vinne na naamini mambo yatakuwa shwari, na bado tunaendelea kulishughulikia suala hilo," alieleza Mhe. Samia.

Jarida la Ni Magufuli Tena

2020 - 2025



Limeandaliwa na **TEAM MAGUFULI TENA**